



## **TAARIFA KWA UMMA**

### **BENKI KUU YA TANZANIA YACHUKUA USIMAMIZI WA CHINA COMMERCIAL BANK LIMITED**

Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha sheria namba 56 (1)(g)(i)&(iii) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania imeamua kuchukua usimamizi wa China Commercial Bank Limited kuanzia leo tarehe 19 Novemba 2020.

Uamuzi huu umechukuliwa baada ya kubaini kuwa China Commercial Bank Limited ina upungufu mkubwa wa mtaji kinyume na matakwa ya sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake. Upungufu huu wa mtaji unahatarisha usalama wa sekta ya fedha na pia kuendelea kutoa huduma za kibenki kwa China Commercial Bank Limited kutahatarisha usalama wa amana za wateja wake.

Kufuatia uamuzi huo, Benki Kuu ya Tanzania imeisimamisha Bodi ya Wakurugenzi na Uongozi wa China Commercial Bank Limited kuanzia leo tarehe 19 Novemba 2020. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania imemteua Meneja Msimamizi ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za China Commercial Bank Limited kwa kipindi ambacho itakuwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu. Hivyo, umma unaarifiwa kuwa katika kipindi kisichozidi siku tisini (90) kuanzia siku ya taarifa hii, shughuli za utoaji wa huduma za kibenki za China Commercial Bank zitasimama ili kuipa nafasi Benki Kuu ya Tanzania kutathmini hatua za kuchukua ili kupata ufumbuzi wa suala hili.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuuhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenyewe amana katika mabenki kwa lengo la kuleta ustahimilivu katika sekta ya fedha.

**BENKI KUU YA TANZANIA  
19 Novemba 2020  
[botcommunications@bot.go.tz](mailto:botcommunications@bot.go.tz)**